

Kituo Cha Kupokea cha ESL

Hazelwood Elementary/Lower level, 1325 Bluegrass Avenue, Louisville, KY 40215



Kwa mojiibu wa kanuni za Wilaya shule ya Jefferson County Public School District inahitajika kuwabaini wanafunzi ambao Kiingereza si lugha yao ya asili na ku kisi ujuzi wao ya lugha ya Kiingereza. Kituo Chakupokea cha ESL (ESL Intake Canter) inasidia kwa kusajili na tathmini ya wanafunzi. Kufanya miadi, tafadhali piga **(502) 485-3623**.

Ni muhimu kwa mzazi au mlezi kufwatana na mwanafunzi kuhudhuria kwa miadi.

Zinahitajika hati na maelezo zifuatazo:

- Thibitisho la kuzaliwa (1-94, pasipoti au cheti cha kuzaliwa)
- Anwani (kukodisha, bili yamatumizi ya hivi karibuni)
- Numba ya cheti cha usaidizi ya chakula (kama zinatumika).
- Vitambulisho vya wazazi (kutoka U.S. au nchi ya zamani, leseni ya dereva au kadi ya ubalozi)
- Rekodi /Nakala kutoka shule ya awali (kama ipo)
- Kentucky Medical Examination - Uchunguzi wa Afya ya Kentucky - (Kila shule inahitaji na inao kumbukumbu hizi)
- Kentucky Immunization Certificate - Cheti cha Chanjo Kentucky – (Kila shule inahitaji na inao kumbukumbu hizi)
- Uchunguzi wa mato - Kentucky Vision Examination - (Kuanzia Januari 1 ya mwaka wa kwanza wa uandikishaji)
- Uchunguzi wa meno Kentucky.

Katika Kituo cha kupokea:

- Wa fanya kazi wa Kituo cha ku pokea ambao wanazungumza zaidi la lugha moja wanasaidia katika kujaza fomu za kujiunga na shule.
- Mtoto atafanya mtihani ya lugha ya Kingereza illi kujulikana kama yeye atastahiki kupata huduma za ESL.
- Kushiriki katika ESL ni hiari.
- Kama mwanafunzi ha kufuzu kupata ESL au mzazi atamua kutupilia mbali huduma za ESL, mwanafunzi atarejeshwa kwa shule ya karibu na nyumba yake (itategemea anwani yake) na atawekwa kwenye clasi ambao italingana na masomo yake. Wafanya kazi wa kupokea watampatia mzazi taarifa kuhusu shule za umma za County ya Jefferson.
- Wazazi watakao kukubali huduma za ESL (isipokuwa watoto wa shule ya Chekechea ambao watasajili mapema), wata pokea simu na watapewa taarifa kuhusu upangaji wa shule, habari za basi, kanuni mavazi ya mwanafunzi et.

kuanza Chekechea, mtoto lazima kuwa na umri wa miaka 5 au kabla ya Oktoba 1.

Kwa habari zaidi au kuweka miadi kwa ajili ya usajili na tathmini, ita (502) 485-3623 katikati ya **7:30 asubuhi na 4:30 mchana**.